

HUDUMA YA UTOAJI WA VIBALI VYA MAJI

AINA YA VIBALI VINAVYOTOLEWA NA BODI YA MAJI YA BONDE LA ZIWA VICTORIA

- Kibali cha matumizi ya maji
- Kibali cha kuchimba kisima kirefu
- Kibali cha kutiririsha maji
- Kibali cha kupitisha muundombinu kwenye eneo la mtu mwingine na kwenye chanzo cha maji

Huduma za vibali vingine.

Huduma hii inamwezesha Mwombaji kupata kibali cha kutumia maji kihalali kwa ajili ya matumizi yafuatayo;

1. KIBALI CHA MATUMIZI YA MAJI (WATER USE PERMIT)

- Matumizi ya nyumbani (binafsi au kikundi)
- matumizi ya shughuli za kibiashara (hotel, lodge, pub n.k)
- usambazaji wa maji kwenye Jamii (Mamlaka za Maji, jumuiya za watumia maji)
- kukinga na kuhifadhi maji kwenye Bwawa
- Umwagiliaji mdogo mdogo & mkubwa
- Kilimo-Biashara/kuuza maji
- Kunyweshea Mifugo.
- ufugaji wa Samaki kwa njia ya mabwawa na vizimba.
- matumizi ya Kiwandani
- kufanya usafirishaji wa Vyombo vya majini kwenye maji baridi (Mito na Maziwa)
- Ujenzi (barabara, majengo, reli n.k)
- shughuli za uchimbaji Madini
- uzalishaji wa maji ya kunywa ya chupa
- uzalishaji wa Nishati/Umeme

2. KIBALI CHA KUCHIMBA KISIMA (DRILLING PERMIT)

- Huduma hii inamwezesha Mteja kupata kibali cha kuchimba kisima kirefu

3. KIBALI CHA KUTIRIRISHA MAJITAKA (DISCHARGE PERMIT)

- Yatokanayo na matumizi ya majumbani
- Yatokanayo na shughuli za Viwandani
- Yatokanayo na shughuli za Kilimo/Umwagiliaji

- Yatokanayo shughuli za madini
- Yatokanayo na shughuli za ujenzi wa miundombinu mbalimbali

4. KIBALI CHA KUPITISHA MIUNDOMBINU YA MAJI (EASEMENT PERMIT)

- Huduma hii inamwezesha Mtumia maji kupata msaada wa Kiofisi ili kupitisha miundombinu ya maji kwenye maeneo ya Watu wengine pamoja na vyanzo vya maji.

UTARATIBU WA KUOMBA KIBALI CHA KUTUMIA MAJI JUU NA CHINI YA ARDHI, KUTIRIRISHA MAJI NA KUPITISHA MUUNDOMBINU KWENYE VYANZO VYA MAJI

- Barua ya maombi: Mwombaji anatakiwa kujaza fomu ya maombi na kuwasilisha katika ofisi ya Bodi; ikiambatana na ada ya maombi. Ombi husika, ada hizi hutofautiana kutokana na aina ya matumizi ya maji.
- Ombi hutangazwa kwenye gazeti la serikali na tangazo hilo huwekwa kwenye mbao za matangazo kwa wakuu wa wilaya husika.
- Bodi itaomba maoni kutoka kwa watumiaji wa chanzo hicho ambapo wanaweza kuathirika kama ombi litakubaliwa.
- Pia itaomba maoni kutoka Halmashauri husika. Kwa miradi mikubwa hadi uthibitisho wa Baraza la Taifa la Usimamizi wa Mazingira (NEMC) huitajika kwa ajili ya athari za kimazingira na kijamii.
- Bodi itakagua eneo la chanzo cha kuchukulia maji na kuchukua sampuli ili kujua ubora wa maji hayo.
- Kwa mujibu wa **Sheria ya Usimamizi wa Rasilimali za Maji Na. 11 ya mwaka 2009 na Maboreshoyake Na.8 ya Mwaka 2022** baada ya siku arobaini kupita tangu kuombwa kwa maoni na kutangazwa kwenye gazeti la serikali, ombi linaweza kufikishwa katika kikao cha bodi ya maji ya Bonde.
- Kibali hutolewa kwa maombi yaliyoidhinishwa na kikao cha bodi; Mkurugenzi, ambaye pia ni katibu wa bodi ya maji ya Bonde anaweza kutoa au kutotoa kibali kufuatana na maelekezo ya bodi.
- Kwa maombi yaliyokataliwa, waombaji wana haki ya kukata rufaa kwa Waziri mwenye dhamana na maji.

Muombaji wa Kibali anahitaji kua na Viambatanishi vifuatavyo;

A. MAOMBI YA KIBALI CHA MATUMIZI YA MAJI (APPLICATION FOR WATER USE PERMIT)

- Barua ya maombi
- Ripoti ya uchimbaji kisima, ikionyesha kina (urefu wa kisima) na uwezo wa kisima.

- Ripoti ya uchuguzi wa maji juu ya ardhi (Hydrological Survey Report)
- Ripoti ya maabara, ikionyesha “ubora wa maji”

B. MAOMBI YA KUTIRIRISHA MAJITAKA (APPLICATION FOR PERMIT TO DISCHARGE)

- Barua ya Maombi
- Ripoti ya maabara, ikionyesha kiwango cha maji yanayotupwa (Laboratory Report)
- Leseni ya biashara (Business Licence)
- Leseni ya makazi (Licence of Occupancy/Title Deed)
- Kibali cha ujenzi (Building Permit)
- Kibali cha uzalishaji (Production Permit)
- Kiwango cha uzalishaji (Industry Production Capacity)
- Environmental Clearance Certificate
- Environmental Audit Certificate
- Final Environmental Audit Report

C. MAOMBI YA KUCHIMBA KISIMA (APPLICATION FOR PERMIT TO SINK OR ENLARGE A WELL OR BOREHOLE)

- Ripoti ya Survey (Survey Report)

D. KUOMBA HAKI YA NJIA KATIKA ARDHI (APPLICATION FOR PERMIT FOR AN EASEMENT)

- Kibali cha matumizi ya maji
- Vielelezo vya ardhi ambapo kibali kipo
- Vielelezo vya ardhi ambapo maji yanakwenda
- Maelezo ya uhamishaji wa maji na kazi zitakazofanyika
- Makabrasha/vielelezo vya fidia
- Makubaliano ya pande zote mbili

HUDUMA YA VIBALI VINGINE

1. KUPITISHA MIUNDOMBINU MTONI & KURUDISHA MTO KWENYE NJIA YAKE

Huduma hii inamwezesha Mteja kupata ruhusa ya kupitisha miundombinu mtoni mfaHAKUNA mabomba ya mafuta, maji, madaraja. Pia inamwezesha Mteja kupata ruhusa ya kuondoa madini mchanga mtoni kwa lengo la kulinda kina cha mto na kurudisha mto kwenye njia yake

2. UHAMISHO WA UMILIKI WA KIBALI CHA MAJI

Huduma hii inamwezesha Mteja kubadilisha umiliki wa kibali baada ya kununua mali za Mmiliki wa awali au baada ya Mmiliki wa awali kufariki